



Zodo Miraji Zodo

MKURUGENZI WA TIA KIZIMBANI KWA UHUFUMU UCHUMI

Na Mussa Misalaba, Dar es Salaam

Aprili 4, 2018

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imempandisha kizimbani Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Huduma wa chuo cha Uhasibu Tanzania anayeshughulikia masuala ya Utumishi, Utawala na Fedha, Zodo Miraji Zodo (55), kujibu shtaka la kuhujumu uchumi.

Mshtakiwa amefikishwa kwenye mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Jijini Dar es Salaam leo mbele ya Hakimu Mkuu Mkazi, Thomas Simba, na kusomewa mashtaka na mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Max Ari.

Upande wa mashtaka uliarifu mahakama kuwa katika tarehe tofauti kati ya Mei 1, 2014 na Mei 1, 2016 mshtakiwa, akiwa Dar es Salaam na akiwa mwajiriwa wa Chuo Cha Uhasibu Tanzania katika nafasi ya Mkurugenzi wa Misaada na Huduma alikisababishia hasara Chuo hicho kiasi cha Shilingi 147, 256, 661.53 kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yake kama alivyopaswa.

Mshtakiwa ambaye alikuwa akitetewa na wakili wa kujitegemea, Jamhuri Johnson, amekana shtaka dhidi yake na upande wa mashtaka umeiambiia mahakama kuwa uchunguzi wa kesi hii haujakamilika na uliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kesi kutajwa.

Wakili Johnson aliiomba mahakama itoe dhamana kwa mshtakiwa kwa kuwa shtaka hili linadhaminika na wakili wa Jamhuri aliiomba mahakama izingatie masharti ya Kifungu namba 148(5e) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 toleo la mwaka 2002, kinachoweka masharti ya dhamana kwa kesi inayohusiana na fedha.

Baada ya hoja za upande wa utetezi na mashtaka hakimumu Simba alitoa masharti ya dhamana kwa mshtakiwa ambapo alitakiwa kuwasilisha mahakamani hati ya kusafiria, kutotoka nje ya Dar es Salaam bila kibali cha mahakama, kuwa na wadhamini wawili ambao mmoja awe mtumishi wa Serikali na mwingine atoke sehemu yoyote .

Masharti mengine ya dhamana ni kuwa kila mdhamini asaini bondi ya Shilingi 73,000,700 /= na mmja wao alipe fedha taslimu Shilingi 73,000,700/= au kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani isiyopungua Shilingi 147, 256, 661.53.

Kesi imeahirishwa hadi Aprili 16, 2018 itakapokuja kwa kutajwa na mshtakiwa yuko nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana kwa kuwasilisha hati ya kusafiria, kuwa na wadhamini wawili ambao wote ni watumishi wa serikali waliowasilisha hati ya nyumba yenye thamani ya Shilingi milioni 178 na walisaini bondi ya Shilingi 73,000,700/=.